

**TANGAZO LA SERIKALI NA.....**

**LA TAREHE: .....**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) 1982  
SHERIA NA. 7 YA 1982**

**Zimetungwa chini ya kifungu Na. 148**

**SHERIA NDOGO (MATUMIZI NA ULINZI WA JOSHO; MBAUTI NA LAMBO)  
ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI, 2008**

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo (matumizi na Ulinzi wa Josho Mbauti na Lambo) za Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Jina
2. Sheria ndogo hizi zitaanza kutumika mara zitakapoidhinishwa na Waziri Mwenye dhamana na Serikali za Mitaa Muda wa kuanza kutumika
3. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Mahali itatumika
4. Katika sheria Ndogo hizi:-  
"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Tafsiri na maneno

"Josho" maana yake ni sehemu maalum iliyochimbwa na kujengwa rasmi ili kuweza kuhifadhi dawa iliyochanganywa na maji kwa ajili ya kuogeshea mifugo kwa madhumuni ya kuua kupe na wadudu wengine waenezao magojwa ya mifugo kama vile Ndigana kali;

"Lambo" ni eneo lililochimbwa na kujengewa tuta na utoro ili kuweza kuhifadhi maji yatiririkayo na kutumia kwa binadamu;

"Mbauti" ni birika la maji lilijengwa kwa saruji kwa ajili ya kunyweshea mifugo na hupata maji yake kutoka kwenye lambo.

5. Kila mwenye mifugo ndani ya eneo la kilometa nane (8) toka kwenye joshlo linalofanya kazi atatakiwa na sherika ndogo hizi kuogesha ng'ombe, mbuzi, na kondoo na mifugo aina nyingine kama inavyoagizwa na Afisa Mifugo au Afisa muidhinishwa na kwa kuzingatia taratibu na ratiba zitakazotangazwa.
6. Mtu yejote au asasi au mfanyakishara akiwa mmiliki wa Josho atatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri na atatakiwa kutangaza wazi ada ya kuogesha mifugo.

7. Kila mfugaji atalazimika kulipia ada ya uogeshaji kama itakavyopangwa na mmiliki wa josho katika eneo lake.
8. Kila atakayesafirisha mifugo ikiwa ni kwa sababu ya biashara au sababu nyingine atalazimika kuogesha mifugo yake kwenye Josho lililo karibu na mahali alipoitoa au alipoinunua na kwa vyovoyote vile anatakiwa na sheria ndogo hizi asiingize wala kupitisha au kutoa Mifugo toka Wilaya ya Rufiji kwenda wilaya nyingine bila kuogesha mifugo hiyo.
9. Mifugo yote italazimika kunyweshwa maji kwenye mbauti kwa Maeneo yenye majosho na mbauti. Ni marufuku kwa mifugo kunyweshwa kwenye malambo moja kwa moja.
10. Ni marufuku kujenga, kulima, kukata miti, kuchoma moto na mkaa, kuwinda na kuchunga mifugo ndani ya mita 300 (mia tatu) kutoka kwenye Lambo.
11. Ni marufuku kujenga, kulima mazao mbalimbali na kuchoma moto ndani ya mita 300 (mia tatu) kutoka kwenye josho la Mbauti.

Nembo na Mhuri wa Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji umebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 06 Septemba, 2008  
Mhuri umebandikwa mbele ya: -

**AZIMINA MBILINYI  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI WILAYA RUFIZI**

**KHATIBU CHAUREMBO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA RUFIZI**

**NAKUBALI:**

**MIZENGO PINDA (MB)  
WAZIRI MKUU  
JAMBURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DODOMA**

**TAREHE .....2008**

**TANGAZO LA SERIKALI NA ..... LA TAREHE .....**  
**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) 1982**  
**SHERIA NA. 7 YA 1982**

**Zimetungwa chini ya kifungu Na. 148**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI**  
**(UDHIBITI NA UTUNZAJI WA MIFUGO) 2008**

1. Sheria ndogo hizi ziitwe Sheria Ndogo (Udhibiti na utunzaji Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ya 2008 na zitaanza kutumika tarehe ya kusainiwa na Waziri mhusika.
2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo la **Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji**.
3. Katika sheria ndogo hizi  
**'Halmashauri'** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji;

**'Wilaya'** Maana yake ni eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Kisheria.

**'Mifugo'** maana yake ni ng'ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe, farasi, punda, mbwa, bata, kuku, paka na wanyama wote wanaofugwa

**'Banda'** au Boma la Mifugo maana yake ni eneo lolote ambalo limejengwa kwa ajili ya kuhifadhi mifugo;

**'Makazi'** maana yake ni nyumba yoyote wanayoishi watu hata kama ni ya muda.

**'Afisa Muidhiniwa'** maana yake ni Afisa/Kilimo au Afisa ye yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kutekeleza sheria ndogo hizi.

**'Kufuga mifugo'** maana yake kumiliki au kutunza mifugo kwa madhumuni yoyote yaliyo halali

**'Shamba'** maana yake ni kipande cha ardhi kinacholimwa mazao ye yeyote ya kilimo kabla wakati na baada ya mavuno ya mazao hayo;

**'Mtu anayefuga mifugo'** maana yake ni mtu ye yeyote anayemiliki au kutunza mifugo, ikiwa ni pamoja na mtumishi wake au jamaa yake anayetunza mifugo hiyo.

- (2) Mifugo yote inatakiwa kubakia na kulishwa ndani ya banda au boma mahali ambapo maeneo ya malisho hayajatengwa kwa dhumuni hilo (zero grazing)
- (2) Wafugaji wote wanaofuga ndani (zero grazing) watafuata utaratibu ufuataao:-
- i. Wafugaji wanaoishi katika maeneo ya 'Low Density Area' wataruhusiwa kufuga ng'ombe wasiozidi wanane (8);
  - ii. Wafugaji wanaoishi katika maeneo ya kawaida (high density area) watafuga ng'ombe wasiozidi wawili (2).
- (4) Katika sehemu za ufugaji huria Halmashauri itakuwa na jukumu la kupima na kutenga maeneo ya ufugaji.
- (5) Wafugaji wote wa mbwa wataruhusiwa kufuga Mbwa wasiozidi wane (4). Mbwa watafungwa kuanzia saa 12.00 asubuhi na kufunguliwa saa 2.00 usiku.
- (6) Mifugo yote inatakiwa inyweshwe maji kwenye Mbauti ambazo zitajengwa na Halmashauri ya Wilaya au Serikali ya Kijiji.
- (7) (1) Ili kudhibiti magonjwa yanayosababishwa na kutoogeshwa kwa mifugo, mifugo yote inayostahili kuogeshwa inatakiwa iogeshwe si chini ya mara moja kwa wiki.
- (2) Mbwa, paka, ngedere wanaofugwa ni lazima wachanjwe chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa angalau mara moja kwa mwaka.
- (3) Wanyama wote wanaofugwa lazima wachanjwe chanjo mbali mbali dhidi ya magonjwa yanayoambukiza (contagious disease) mara moja kwa mwaka.
- (8) (1) Mifugo yote kutoka na kuingia ndani ya wilaya itatakiwa kupata Kibali kutoka kwa Mganga wa mifugo aliyethibitishwa na Wasafirishwe kwa kutumia gari moshi au motokaa (gari)
- (2) Mifugo kutoka kwa Mganga wa mifugo wa Tarafa au wa Kata inayohusika na isafirishwe kwa kutumia magari au gari moshi.
- (9) (1) Mtu yejote atakayechunga au kulisha mifugo yake nje ya sehemu Zilizotengwa kwa ajili hiyo au kunywesha maji nje ya Mbauti zilizo Jengwa kwa ajili hiyo atakuwa ametenda kosa dhidi ya sheria ndogo hizi.
- (2) Mtu yejote atakayezidisha idadi ya mifugo katika sehemu zilizotajwa kisheria atakuwa ametenda kosa dhidi ya Sheria Ndogo hizi.

- (3) Mtu yeyote atakayefuga mbwa zaidi ya wanne au kufungua mbwa kabla ya saa 2.00 usiku atakuwa ametenda kosa
  - (4) Mtu yeyote atakayekataa kuchanja mbwa, ngedere na paka dhidi ya kichaa cha mbwa mara moja kwa mwaka atakuwa ametenda kosa dhidi ya sheria ndogo hizi.
  - (5) Mtu yeyote atakayekataa kuchanja mifugo yake chanjo mbali mbali dhidi ya sheria ndogo hizi.
  - (6) Mtu yeyote atakayekataa kuchanja mifugo yake chanjo mbali mbali dhidi ya magonjwa yanayoambukiza (contagious diseases) mara moja kwa mwaka atakuwa ametenda kosa dhidi ya sheria ndogo hizi.
  - (7) Mtu yeyote atakayesafirisha mifugo bila ya kibali kutoka kwa mganga wa mifugo aliyethitishwa na bila ya kutumia usafiri wa gari au gari moshi atakuwa ametenda kosa dhidi ya sheria ndogo hizi.
  - (8) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume au atayekosa kutii sheria ndogo hizi atakuwa ametenda KOSA na atakapopatikana na HATIA atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita (6) au kupewa adhabu zote mbili yaani faini na kifungo kwa pamoja.
  - (9) Ni marufuku mtu anayefuga mifugo kuingiza, au kulisha mifugo hiyo katika shamba la mtu mwingine bila ya idhini ya mwenye shamba
  - (10) Mtu atakayekiuka sheria ndogo hizi, akipatikana na hatia atalipa faini ya Tshs. 100,000/= au kifungo cha miezi 12 jela, au kutumikia adhabu zote mbili, kulipa faini na kifungo.
- 
- (10) (1) Mtu atakayeingiza na au atakayelisha mifugo katika shamba la mtu Mwingine atamlipa fidia, mwenye shamba hilo kwa uharibifu Utakaokuwa umefanywa, pamoja na adhabu inayotolewa katika Sheria ndogo ya 8 ya sheria ndogo hizi.
  - (2) Fidia itakayolipwa chini ya sheria ndogo hizi itakuwa ni thamani ya bei ya soko ya mazao yaliyoharibiwa kama yatakavyokuwa yametathminiwa na Afisa Muidhinishwa.

## **JEDWALI**

**RUHUSA Y KUPTISHA NG'OMBE, MBUZI, KONDOO, NGURUWE, FARASI,  
PUNDA N.K.**

**Ruhusa itatolewa kwa:** .....

**Kwa ajili ya kupitisha** .....

**Katika Kata ya** .....

**Wilaya ya** .....

**Maelezo** .....

.....

.....

**Nakala:** .....

**Tarehe:** ..... **Wakatabahu** .....

Nembo na mhuri wa Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uliobandikwa kwenye sheria hii ndogo kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmasharui uliofanyika tarehe..... 2008.

**AZIMINA MBILINYI  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI WILAYA RUFIFI**

**KH. CHAUREMBO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA RUFIFI**

**NAKUBALI .....**

**Mhe. Mizengo Pinda (MB)  
WAZIRI MKUU  
JAMBURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DODOMA**

**TAREHE .....2008**

**TANGAZO LA SERIKALI NA..... LA TAREHE: .....**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) 1982  
SHERIA NA. 7 YA 1982**

**Zimetungwa chini ya kifungu Na. 148**

**SHERIA NDOGO ZA KUFUFUA NA KUTUNZA MASHAMBA YA ZAO LA  
KOROSHO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI, 2008**

1. Sheria ndogo hizi zitaitwa sheria ndogo ya kufufua na kutunza mashamba ya zao la korosho ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji za mwaka 2008 na zitaanza kutumika mara zitakapoidhinishwa na kutiwa saini na Waziri mwenye dhamana na serikali za mitaa.
2. Katika sheria ndogo hizi:  
“Halmashauri” maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

“Mwenye shamba” maana yake ni mtu binafsi, kikundi, au Kampuni ambayo ina miliki shamba kwa sheria za mila, serikali au vinginevyo.

‘Mtu mzima’ maana yake ni mkazi yeote au mwana kaya mwenye umri kuanzia miaka 18 katika kijiji au eneo lolote la Wilaya hii.

“Shamba” maana yake ni Ardhi inayolimwa/iliyolimwa zao la korosho lenye hati ikiwa ni pamoja na shamba linalomilikiwa kimila.

“GRN” ni namba ya usajili ya mkulima wa korosho anayopewa baada ya kusajili kuwa ni mkulima wa korosho.

“Gunia” maana yake ni gunia la mkonge au jute litakalotumika kuhifadhiwa korosho.

“Magugu” maana yake ni miti na nyasi au mimea ambayo huota na kuathiri ukuaji au ustawi wa mikorosho au matunda yake.

“Miche bora” maana yake ni miche iliyozalishwa kutokana na mbegu bora.

“Mnunuzi” maana yake ni mnunuzi wa korosho

“Mbegu bora” maana yake ni mbegu zinazozalishwa na vituo vya uzalishaji wa mbegu za korosho vilivyo chini ya kituo cha utafiti wa kilimo.

"Kupalilia" maana yake ni kukata miti na kuchimbua visiki pamoja na kulima nyasi mwaka hadi mwaka au kila inapohitajika kufanya hivyo.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji Wilaya pamoja na watumishi wote wa idara ya Kilimo, mifugo, ushirika na Masoko na Maafisa Waendaji wa Kata na yeoyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi wa Wilaya kwa madhumuni ya sheria ndogo hizi.

"Afisa Kilimo" maana yake ni mtumishi wa halmashauri ya Wilaya anayefanya kazi ya taaluma ya kilimo.

"Kipimo rasmi" maana yake ni kipimo cha kilogramu na au tani.

3. (1) Kila mkazi wa kijiji au maeneo yoyote ya halmashauri ya wilaya Bagamoyo mwenye umri wa miaka kuanzia 18 anatakiwa alime shamba la korosho, hii ni kwa vijiji na maeneo zao la korosho linapostawi vizuri kitaalamu, na kwa wakazi ambao hawana kazi ya ofisini inayotambulika.  
  
(2) Endapo kuna kaya yenyewe vijana wenyewe umri wa miaka 18, wanakaya hao wanapaswa walime mashamba yao ya korosho yao wenyewe hata kama bado wanaishi na wazazi wao.  
  
(3) Wajibu wa kulima shamba la korosho kwa kila mkazi wa Halmashauri ya wilaya ya Rufiji ni kuanzia ekari moja  
  
(4) Kila mwazilishi wa shamba jipya la korosho anapaswa kutumia mbegu na au miche bora.
4. (1) Kila mwenye kumiliki shamba la mikorosho katika eneo lililoko ndani ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji analazimika kulitunza shamba hilo kwa kupalilia magugu kila mwaka na ifikapo tarehe 31 Julai, kila mwaka shamba la mikorosho lolote liwe limepaliliwa.  
  
(2) Kila mwenye kumiliki shamba la mikorosho ahakikishe kuwa anatumia/ananyunyuzia dawa za kuzuia au kutibu magonjwa mbalimbali ya mikorosho kama itakavyoshauriwa na Afisa Kilimo.  
  
(3) Kila mkazi wa Halmashauri ambaye anamiliki shamba la mikorosho lenye miti michakavu, anapaswa aidha kung'oa miti hiyo na kupanda miche mipywa au kuikata ili iweze kuchipua upya kwa maelekezo atakayopewa na Afisa Kilimo.

**Wajibu wa  
kutunza  
shamba la  
Korosho**

5. (1) Kila Afisa Mtendaji Kata akishirikiana na serikali ya kijiji anawajibika kutunza kumbukumbu za mashamba yote ya mikorosho yaliyomo katika kata yake na atasimamia moja kwa moja utunzaji wa mashamba hayo.  
(2) Afisa Mtendaji wa Kata na serikali ya kijiji watakagua na watatambua mashamba ambayo hayapaliliwi na wenye mashamba hayo ili wachukuliwe hatua.
6. (1) Endapo itabainika kuwa shamba la mikorosho limeingiliwa na wadudu waharibifu au magonjwa itakuwa ni jukumu la mwenye shamba kutoa taarifa mara moja kwa Afisa Kilimo au Afisa Muidhiniwa.  
(2) Mwenye shamba atawajibika kuchukua hatua za kuangamiza wadudu waharibifu au kutibu magonjwa kama atakavyokuwa ameelekezwa na Afisa Kilimo au Afisa Muidhiniwa ili kuponyesha mikorosho yake au kuzuia uenezaji wa wadudu waharibifu na magonjwa kwenye mashamba mengine.
7. Afisa Kilimo au Afisa Muidhiniwa anaweza kwa wakati wowote unaofaa kuingia shambani na kukagua hali ya shamba na ustawi wa mikorosho.
8. Mwenye shamba atalitunza shamba lake, na iwapo hajafanya hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu, taarifa ya mwezi mmoja itatolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwenye magazeti yanayosomeka na watu wengi na pia mahali shamba lilipo na kumtaka mwenye shamba ajitokeze na kupalilia shamba lake katika muda wa miezi miwili tangu tarehe ya Tangazo na akishindwa kutekeleza maagizo hayo atakuwa ametenda kosa.
9. Mtu yeyote:
  - (1) Atatekeleza maelekezo au ushauri wa Afisa Kilimo au Afisa Muidhiniwa katika kutunza shamba lake au katika kuangamiza wadudu na kutibu magonjwa kipindi utakapotolea;
  - (2) Atatoa taarifa ya kuwepo wadudu au magonjwa yalioingia shambani kwake;
  - (3) Hatapalilia shamba lake kwa kuchoma moto;
  - (4) Atapalilia shamba lake katika muda uliowekwa na sheria;
10. (1) Kila mkulima na wajibu wa kuvuna korosho katika shamba lake mara tu zinapokuwa tayari.

Uvunaji wa korosho ni ule tu wa kuokota tunda la korosho ambalo limeanguka lenyewe baada ya kukomaa.

- (2) Ni marufuku kwa mtu yeote kuangusha/kutungua tunda la mkorosho kwa lengo la kulazimisha kuangua/kuvuna
- (3) Mara baada ya kuokota matunda ya korosho ambayo yameanguka lenyewe, mkulima anapaswa kutenganisha korosho na tunda
- (4) Baada ya utenganisho wa korosho na matunda, mkulima anapaswa kukausha korosho zake juani ka kutumia vifaa vya kuanikia visafi.
- (5) Baada ya korosho kukauka mkulima napaswa kutenga korosho zake kwa madaraja ambayo ni la kwanza na la pili na kuzihifadhi korosho zake zikiwa katika madaraja hayo.

**Kuhifadhi  
korosho**

11. (1) Kila mkulima napaswa kuhifadhi korosho zake ambazo zimetengwa kwenye madaraja ya kwanza na pili katika magunia ya mkonge au “jute”

- (2) Ni marufuku kuhifadhi korosho kwenye vifaa visivyopitisha hewa kama mifuko ya plastiki au magunia ya “Viroba”
- (3) Korosho zote zilizo kwenye magunia zihifadhiwe kwenye maghala yanye sifa zifuatazo:-
  - i) Lenye uwezo wa kuingiza hewa ya kutosha
  - ii) Lisilovuja na kupitisha maji wakati wa mvua na;
  - iii) Lenye reli za kubebea magunia ya korosho (Pallets)

**Uuzaji wa  
Korosho**

12. Mkulima wa korosho anapaswa kuza korosho zake kwenye kituo cha kuuzia korosho (Buying Post) ambacho kimesajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushauriwa na Halmashauri ya Wilaya.

13. Mkulima wa korosho atauza korosho zake kwa mnunuzi mwenye leseni ya ununuzi iliyotolewa na bodi ya Korosho Tanzania na kibali na leseni ya ununuzi huo atakayopewa na Halmashauri ya Wilaya.

14. (1) Mnunuzi atalazimika kutoa maelezo kamili ya anuani yake ya posta, na namba ya simu na mahali ilipo ofisi au makazi kwa lengo la kupata mawasiliano ya uhakika.
- (2) Mnunuzi asiyekuwa na anuani kamili au mahali ofisi ilipo hataruhusiwa kupata kibali cha kununua korosho.

- (3) Mnunuzi kabla ya kununua korosho ataomba kibali cha ununuzi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Bagamoyo; na
- (a) Kibali kitakachotolewa kitaonyesha kiasi cha tani zinazohitajika na zilizonunuliwa, pamoja na namba ya stakabadi ya ushuru aliolipita na;
  - (b) Kibali kitakachotolewa kitakuwa cha tani 100 (mia moja) na kuendelea na baada ya mnunuzi kumaliza kununua tani zilizoorodheshwa kwenye kibali atawajibika kuomba kibali kingine; na
  - (c) Mnunuzi baada ya kufunga mkataba na Halmashauri na kupata kibali cha ununuzi atatakiwa kulipia ushuru wa korosho wa kuanzia tani 100 (mia moja) na kuendelea.
15. Mnunuzi atanunua korosho za wakulima katika kituo cha ununuzi kilichosajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania na siyo kufuata wakulima majumbani, au na mashambani.
16. Ununuzi wa korosho utaana kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni ya siku moja
17. Mnunuzi, wakati wa ununuzi ataandika bei ya madaraja yote ya korosho ili kila muuzaji aelewé bei ya daraja la korosho analouza.
18. Mnunuzi atatumia kapani iliyokaguliwa na Maafisa Mizani/Vipimo vywa wanunuzi.
19. Mnunuzi wa korosho atanunua korosho kwa mkulima aliysajiliwa kwa kukiri namba ya mkulima (GRN)
20. Mnunuzi ataweka kumbukumbu sahihi za ununuzi wa korosho kadri atakavyohitajika na Bodi ya Korosho Tanzania na Halmashauri ya Wilaya.
21. (1) Mnunuzi wa korosho wakati wa kununua korosho atatumia kipimo rasmi kupimia korosho hizo.
- (2) Mnunuzi asimpe mtu mwingine au kampuni kibali chake au kutoa vivuli (Photostat copies) na kugawia wengine.
- (3) Mtu yeyote au kampuni isinunue korosho bila ya kwanza kusajiliwa na bodi ya Korosho Tanzania (CBT)
- (4) Mnunuzi atanunua korosho baada ya kwanza kupata kibali cha ununuzi kitakachotolewa na Halmashauri ya Wilaya.

**Usafirishaji  
wa korosho  
kuelekea  
Bandarini au  
Viwandani**

**Kosa na  
Adhabu**

- (5) Mnunuzi anayedaiwa kodi ya ushuru wa misimu uliopita atalipa kwanza deni lake hilo kabla ya kupata kibali cha kununulia korosho kwa msimu unaofuata. Bila ya kutimiza sharti hilo Mnunuzi hatakubaliwa kununua korosho.
  - (6) Mnunuzi atatumia vipimo vya uzito vya Kilogramu/tani tu.
  - (7) Mnunuzi atalipwa kwa Halmashauri ushuru kabla ya kununua korosho.
22. Kila mnunuzi wa korosho anapaswa kusafirisha korosho alizozinunua akiwa na nyaraka muhimu za ununuzi wa korosho hizo ambazo PDN ya CBT, na kibali cha kununulia na cha kusafirishia korosho kutoka Halmashauri.
23. Mnunuzi, au mtu yejote atasafirisha korosho kuanzia muda wa saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni ya siku moja.
24. (1) Mtu yejote atakayetenda au kutotenda, kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi laki mbili (Ts. 200,000/=) au kifungo cha jela kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.
- (2) Endapo mtu atapatikana na hatia ya kuvunja sheria ndogo ya 8 ya sheria ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumnyang'anya shamba hilo husika kwa kufuata sheria husika.

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uliobandikwa humu kwa kufuata Azimio  
lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri hiyo ulioitishwa vilivyo na kufanyika  
mnamo tarehe .....mwezi .....2008

Muhuri umebandikwa mbele ya .....

**AZIMINA MBILINYI  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI WILAYA RUFIFI**

**KH. CHAUREMBO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA RUFIFI**

**NAKUBALI .....**

**Mhe. Mizengo Pinda (MB)  
WAZIRI MKUU  
JAMBURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DODOMA**

**TAREHE .....2008**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) 1982  
SHERIA NA. 7 YA 1982**

**Zimetungwa chini ya kifungu Na. 148**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI SHERIA NDOGO YA KILIMO NA  
MAZAO YA MWAKA, 2008**

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za kilimo ya mazao za Halmashauri ya wilaya ya Rufiji za mwaka 2008 na zitaanza kutumika tarehe ya kusainiwa na Waziri.
2. Katika sheria ndogo hizi:-

“Halmashauri” ina maana ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

“Afisa Kilimo” ina maana kuwa ni mtu yejote aliye katika Utumishi wa Serikali ambaye ameteuliwa na Afisa Kilimo.

“Afisa Muidhiniwa” ina maana ni mtu yejote aliyeteuliwa na Halmashauri kwa madhumuni ya sheria ndogo hizi.

“Mazao ya Chakula” ina maana ni Mahindi, Mpunga, Muhogo, Mtama, Viazi vitabu, na jamii ya mikunde n.k.

“Mazao ya Biashara: ina maana ni Pamba, Korosho, Nazi, Ufuta, Alizeti, Michungwa, Midimu, Milimau, Mibalungi na Mananasi n.k.

“Mdudu wa mmea harabu” ina maada mududu yejote au mmea wowote ambao huweza kuleta madhara kwa mimea au mazao au majani yaliyoko kando kando yake.

“Mkazi” ina maana ni mtu yejote ambaye kwa kawaida anakaa katika eneo lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri lakini halichanganyi mtu yejote;

- (a) Ambaye umri wake ni chini ya miaka kumi na nane;
- (b) Ambaye umri wake ni zaidi ya miaka hamsini
- (c) Ambaye hawesi kufanya kazi kwa sababu ya maradhi uzee na kutojimudu
- (d) Ambaye ni mfanyakazi.

3. Kila mkazi anayemiliki ardhi kwa mujibu wa sheria za kienyeji zinazohusu umilikaji wa ardhi, atalima na kutunza, eneo lisilopungua ekari mbili za mazao ya chakula yanayostawi na kuhimili hali ya hewa na udogo ya sehemu husika na kama itakavyo elekezwa na HALMASHAURI

4. Afisa Muidhiniwa anaweza kwa wakati wowote unaostahili kuingia kwenye ardhi yejote ya kilimo kwa madhumuni ya kukagua ili kuhakikisha kuwa masharti ya sheria ndogo hizi yanafuatwa.
5.
  - (i) Kulingana na sheria ndogo hizi ni marufuku kwa mtu yejote kung'oa, kuunganisha, kuharibu na kusababisha ing'olewe iangushwe au iharibiwe mimea yejote iliyolimwa na kutunzwa kwa kufuata masharti ya sheria ndogo hizi ila kwa madhumuni ya kuendeleza kilimo au kwa kuhifadhi na kuendeleza mazingira.
  - (ii) Kulingana na sheria ndogo hizi kila mkazi atatakiwa kuhakikisha kuwa anacho chakula cha kutosha kwa mwaka mzima, na iwe ni marufuku kuuza, kutumia mazao ya chakula na biashara kinyume na madhumuni yaliyopo.
6. Mtu yejote atakayekwenda kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na **HATIA** atatozwa faini ya shilingi za Kitanzania elfu Hamsini au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au kupewa adhabu zote mbili, faini na kifungo.

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uliobandikwa humu kwa kufuata Azimio  
lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri hiyo ulioitishwa na kufanyika  
mnamo tarehe .....mwezi .....2008

Muhuri umebandikwa mbele ya .....

**AZIMINA MBILINYI  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI WILAYA RUFIFI**

**KH. CHAUREMBO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA RUFIFI**

**NAKUBALI .....**

**Mhe. Mizengo Pinda (MB)  
WAZIRI MKUU  
JAMBURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DODOMA**

**TAREHE .....2008**

**G. N. NO. ....PUBLISHED ON .....**  
**LOCAL GOVERNMENT FINANCE ACT, 1982**  
**ACT NO. 9 OF 1982**  
**(Made under Section 7)**

**THE RUFIDI DISTRICT COUNCIL**

**TRANSPORT AND TRANSPORTATION (FEES AND CHARGES) BY – LAWS, 2008**

1. These By-Laws may be cited as the Rufiji District Council Transport and Transportation (Fees and charges), By-Laws, 2008 Title
2. These By-Laws shall be deemed to have come into effect on the date of Commencement approval by the Minister responsible.
3. These By-Laws shall apply throughout the area of jurisdiction of Rufiji District Council. Application
4. These By-Laws unless the context requires otherwise: Interpretation

**“Bus Stand”** means any bus stop or station or parking where passengers board and embark from any vehicles from different areas and includes all areas designated for that purpose within Rufiji District.

**“Council”** means the Council of Rufiji District established pursuant to the Local.

**“Authority”** means the Council of the Rufiji District established pursuant to the Local Government. (District Authorities) Act No. 7 of 1982

**“Director”** means the executive head of the Council or any authorized Officer of the Council or its agent.

5. (1) There shall be Rufiji Bus stand to be situated at Kibiti Town  
(2) Every Tax, and motor omnibus offering service in transport business shall park at the Town bus stand, and other place to be determined and named by the authority.  
(3) Every omnibus shall park at the Town Bus stand and the owner shall pay the rate as shown in the first schedule below.
6. (1) No passenger vehicle shall use the Town bus stand unless the owner has paid the rated chargeable in the first schedule below.  
(2) No vehicle shall transport luggage unless the owner has paid the rates chargeable under second schedule below:-

**Obligation to Pay Bus Stand fees**

- (3) No vehicle shall do transport or transportation business unless the owner has registered the vehicle with, and has paid the fee to the authority as shown in the third schedule below:
- (4) Vehicle not registered in Rufiji shall pay entrance fee of Tshs. 1,000/= per day.
- (5) No sailing boat (jahazi) shall do transport business unless the owner has registered it with and paid the fee, to the authority as shown in the forth schedule below;

### **FIRST SCHEDULE**

**BY-LAW (6) (1)**

#### **PAYING AND PARKING FEES FOR TOWN BUS STAND (PASSENGER VEHICLES)**

<b>NA</b>	<b>TYPE OF VEHICLE</b>	<b>PAYING FEE CHARGEABLE (TSHS)</b>	<b>NIGHT</b>
1.			
2.	OMIBUSES (Passenger carrying capacity)		
	(i) 5 – 15	700/= per trip	3,000/=
	(ii) 16 – 25	1,000/= per trip	3,000/=
	(iii) 26 – 65	2,000 pe trip	4,000/=

### **SECOND SCHEDULE**

**BY-LAW (6) (2)**

#### **PAYING AND PARKING FEES LUGGAGE VEHICLES**

<b>NA</b>	<b>TYPE OF VEHICLE</b>	<b>PAYING FEE CHARGEABLE (TSHS)</b>	<b>PARKING FEE (TSHS) NIGHT TIME</b>
1.	1-3 1/4 TONS	500/= PER TRIP	500/= PER DAY
2.	3 1/4 - 10 TONS	1,500/= PER TRIP	1,000/= PER DAY
3.	11 – 15 TONS	2,000/= PER TRIP	1,500/= PER DAY
4.	16 – 25 TONS	5,000/= PER TRIP	2,000/= PER DAY
5.	26 – 40 TONS	10,000/= PER TRIP	5,000/= PER DAY

**THIRD SCHEDULE**  
**BY-LAW (6) (3)**  
**REGISTRATION FEES**

<b>NA</b>	<b>TYPE OF VEHICLE</b>	<b>PAYING FEE CHARGEABLE (TSHS)</b>
1.	TAXI	10,000/= PER ANNUM
2.	Luggage Vehicles (Tonnage)	
	1-3 1/4 TONS	10,000/= PER ANNUM
	3 1/4 - 10 TONS	30,000/= PER ANNUM
	11 – 15 TONS	40,000/= PER ANNUM
	16 – 25 TONS	60,000/= PER ANNUM
	26 – 40 TONS	80,000/= PER ANNUM
3.	<b>Passenger Vehicles</b>  (Passenger carrying capacity)	
	(i) 5 – 15	10,000/= PER ANNUM
	(ii) 16 – 25	15,000/= PER ANNUM
	(iii) 26 – 65	30,000/= PER ANNUM

**FOURTH SCHEDULE**  
**BY-LAW (6) (4)**  
**SAILING BOATS (PARKING/NANGA) PLYING AND REGISTRATION FEES**

<b>NA</b>	<b>TYPE OF BOAT (JAHAZI)</b>	<b>PAYING FEE CHARGEABLE (TSHS) PER DAY</b>	<b>PARKING FEE (TSHS) PER DAY</b>	<b>REGISTRATION (TSHS) PER ANNUM</b>
1.	1-15 metres	500/=	3,000/=	6,000/=
2.	16-30 metres	500/=	5,000/=	10,000/=
3.	31-50 metres	500/=	10,000/=	20,000/=
4.	51-100 metres	500/=	20,000/=	40,000/=

7. (1) Any person who fails or ignores or evades to pay the fees prescribed under By-Law 4 of these By-Laws shall be guilty of an offence and shall be liable for prosecution in courts of law and on conviction shall be liable to a penalty of 50% of the fee and so a fine not exceeding fifty thousand shillings or to imprisonment exceeding twelve months or to both fine and imprisonment.
- (2) Not with standing the provisions of By-Law (1) of this By-Law, the Director may compound the offence under these By-Laws.

Offence and  
Fine

THE COMMON SEAL OF RUFIFI DISTRICT COUNCIL IS HERE UNTO AFFIXED IN PURSUANCE OF THE RESOLUTION PASSED AT A MEETING OF THE COUNCIL DULY CONVENED AND HELD ON THE .....MONTH ..... YEAR 2008 AND THE SAME WAS AFFIXED IN THE

.....  
**AZIMINA MBILINYI  
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR  
RUFIFI**

.....  
**KH. CHAUREMBO  
CHAIRMAN RUFIFI DISTRICT COUNCIL**

**I APPROVE .....**

**HonMizengo Pinda (MP)  
PRIME MINISTER  
UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**DODOMA**

**DATED .....2008**

**TANGAZO LA SERIKALI NA..... LA MWAKA: .....**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982  
SHERIA NA. 9 YA 1982**

**Zimetungwa chini ya kifungu Na. 148**

**SHERIA NDOGO (USHURU WA HUDUMA ITOLEWAYO) ZA HALMASHAURI  
YA WILAYA YA RUFIFI 2008**

**Jina** 1. Sheria ndogo hizi zitaitwa Sheria ndogo (ushuru wa huduma itolewayo) ya Halmashauri ya Wilaya Rufiji 2008

**Kutumika** 2. Sheria ndogo hizi itaanza kutumika mara tu itakapoidhinishwa na Waziri.

**Eneo la  
kutumika** 3. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

**Tafsiri** 4. "Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

"Ushuru wa Huduma" maana yake ni tozo la asilimia kwa mapato ambayo Kampuni, shirika, taasisi, kiwanda, karakana inapata kutoka kwa wateja wake.

"Afisa Mteule" maana yake ni Afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia na kukusanya ushuru huu wa Huduma kulingana na sheria ndogo hizi.

"Kipindi cha mahesabu" ni kipindi au muda au wakati ambao shirika, kampuni, taasisi, kiwanda, karakana na mashamba linafanya au kufunga mahesabu yake biashara.

"Mahesabu" maana yake "assessment" au mahesabu au ya ziada ya ushuru wa huduma yaliyofanywa chini ya sheria ndogo hizi.

“Walipaji” (Levy payers) wa ushuru huu kwa mujibu wa sheria ndogo hizi maana yake Kampuni yejote iliyosajiliwa chini ya sheria ya kampuni, patinashipu au usajili wa Kampuni za miliki wamoja n.k. ambayo inafanya shughuli za kiuchumi kama vile Taasisi, kiwanda, shirika, karakana, bidhaa za viwanda au mashamba, ugawaji wa bidhaa au utoaji huduma au biashara ikiwemo uingizaji wa bidhaa au huduma kutoka nchi za nje kwa ajili ya kuuza.

“Mkusanyaji” maana yake Afisa Mteule au Wakala (Levy collector) aliyejeteuliwa kukusanya ushuru toka kwa Mlipaji au walipaji.

## **SEHEMU YA PILI**

**Jinsi ya kutoza  
ushuru huu**

5. Ushuru huu utatozwa na kukusanya kutoka kwa walipaji (levy payers) au mawakala wote waendeshao shughuli zao ndani ya Halmashauri katika kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo au makusanyo au mapato yaliyopatikana kwa shughuli zote ikiwemo uzalishaji (manufacturing), usindikaji (Processing), Kilimo, ugawaji wa bidhaa, utoaji wa huduma, Biashara, uingizaji wa bidhaa au huduma toka nje ya nchi yetu kuja ndani ya eneo lillio chini ya mamlaka ya Halmashauri.

6. Ili kufahamu mauzo au mapato ambayo mlipaji anayapata au kukusanya mkurugenzi au afisa mteule atamwandikia mkusanyaji ikimtaka aandae vipengele (full particulars) za shughuli zake za kiuchumi ikiwemo idadi (units) na thamani ya fedha ya bidhaa au huduma aliyouza, kugawa, kuingiza toka nje ya nchi kwa madhumuni ya shughuli za kibashara na taarifa yake ya fedha (financial statement) ndani ya muda muafaka lakini si chini ya siku thelathini (3) baada ya notisi hiyo.

**Taarifa yenye  
vipengele vyote  
(Particulars) vya  
shughuli**

7. Mkurugenzi anaweza kumteua Afisa Mteule kuingia ndani ya eneo, jumba, karakana ofisi au stoo ya Mlipaji kwa nia ya kufanya mahojiano, majadiliano, upekuzi na ukaguzi wa mahesabu katika vitabu vya mlipaji kama atakavyoona inafaa ili kuona uwajibikaji wa kweli (True liability) wa Mlipaji.

**Uwezo wa kuingia  
katika eneo la  
“Mlipaji”**

8. Mkurugenzi anaweza kutoa Notisi ya Maandishi akimtaka mlipaji au mkusanyaji kukabidhi kumbukumbu za shughuli vitabu vya mahesabu ya fedha, taarifa ya fedha (mizania au Financial statement) na taarifa au Particulars zingine kama

**Kuwasilisha**

atakavyoona inafaa kwa nia ya kupata taarifa ya mahesabu (assessment) au makusanyo ya ushuru wa huduma.

**Mahudhurio**

9. Kwa nia ya kupata habari chini ya sheria ndogo hizi. Mkurugenzi anaweza kumtaka yeyote kuja kwake au kuja mbele ya Afisa Mteule mahali popote atakapopatikana yeze Mkurugenzi.

**Wajibu wa mkusanyaji wa ushuru**

10. Kila mkusanyaji ushuru au Afisa Mteule au Kampuni anaweza kuteuliwa kuwa Mkusanyaji na atawajibika kutayarisha taarifa (return) katika muda utakaopangwa na Mkurugenzi na kama ilivyoainishwa na Mamlaka na atawajibika kufanya yafuatayo:-

- (a) Kuwasilisha taarifa (return) kwa mkurugenzi au kwa Afisa Mteule
- (b) Kukabidhi ushuru alioukusanya kwa Halmashauri katika muda uliopangwa.

**Muda wa kuwasilisha au kulipa ushuru wa mwisho**

11. (1) Kila mlipaji au mkusanyaji atakabidhi Taarifa ya mwisho (Final Return) kwa Halmashauri ndani ya miezi mine kutoka mwisho wa mahesabu ya fedha (Accounting Period) ikionyesha jumla ya mapato au makusanyo na kulipa ushuru kwa mkupuo mmoja (one instalment)

- (2) Mlipaji au mkusanyaji anapowasilisha taarifa (Return) kwa Afisa Mteule au Mkurugenzi anaweza; kuikubali taarifa (Return) na kuipigia mahesabu (Asses) kama inavyoonyesha au;

- (a) Kama ana sababu nzuri za kumfanya aamini kuwa taarifa (Return) siyo ya kweli na kusahihisha na kuamua kulingana na uamuzi wake, kiasi cha makusanyo/mapato ya mlipaji na kupiga mahesabu kulingana na inavyoonekana.

**Malimbikizo ya ushuru usiolipwa**

12. Kama kuna ushuru wa huduma ambao haujalipwa baada ya muda uliopangwa na sheria ndogo hizi, basi mlipaji atawajibika kulipa limbikizo ya asilimia moja nukta tano (1.5%) kwa mwezi bado pamoja na kiasi anachodaiwa na kulipwa pamoja yaani kwa mkupuo mmoja.

## **SEHEMU YA TATU KOSA NA ADHABU**

**Kuishindwa  
kutekeleza  
matakwa ya  
notisi**

13. Mtu Kampuni au Taasisi yeote bila sababu ya maana:-

- (a) Akishindwa kukabidhi taarifa yote ya kweli kama itakavyotamkwa na sheria ndogo hizi, au
- (b) Akishindwa kukabidhi taarifa (return nyaraka na habari ua Particulars ambazo zilitakiwa kuletwa au kuwasilishwa kwa Mkurugenzi katika muda uliopangwa na sheria ndogo hizi, au
- (c) Akishindwa kutunza kumbukumbu, vitabu au mahesabu ya fedha kulingana na sheria ndogo hizo au
- (d) Atashindwa kutoa kumbukumbu na nyaraka ili kupitiwa au kupitiwa au kukaguliwa (examination) kulingana na matakwa ya notisi kama ilivyotaka sheria ndogo hizi.
- (e) Ambaye siyo Afisa mteule au siyo mhasibu mteule akijifanya kutayarisha taarifa ya mwanzo au ya mwisho (provisional or final return)

**Kufanya  
taarifa  
(return)  
isiyo sahihi  
au kugushi**

14. Mtu, kampuni au Taasisi yeote bila sababu nzuri:-

- (a) Akitayarisha taarifa (return) ya kugushi kwa kuacha kuingiza mapato au makusanyo ya kweli au kuingiza makusanyo chini (understanding), au
- (b) Akitayarisha taarifa au mizania (statement) ambayo si sahihi kuhusiana na uwajibikaji (liability), au
- (c) Akitoa taarifa au habari (information) isiyo sahihi kuhusiana na kitu au jambo linaloathiri uwajibikaji (liability) kwa ushuru wake au wa mtu mwingine, au
- (d) Akitoa taarifa za uongo (false information) kuhusiana na kitu jambo linaloathiri "Liability" ya ushuru wake au wa mwingine.
- (e) Akitayarisha, kutunda au kutoa mamlaka ya matayarisho au utunzaji wa vitabu vya hesabu za fedha bandia (false books of accounts or other records) au akaruhusu utengenezaji wa vitabu vya hesabu ya fedha (falsification of such books of accounts or records) au;
- (f) Akitumia kugushi au akaruhusu (authorize) matumizi ya nyaraka za kugushi.

(g) Atakuwa ametenda kosa la jinai na hivyo atafikishwa mahakamani na akapatikana na hatia atalipa faini ya shilingi elfu kumi au kifungo cha miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili yaani kifungo na faini.

**Kumzuia Afisa  
mteule au  
Mkurugenzi  
kufanya kazi  
yake**

15. Yeyote katika njia au namna yeyote ile atajaribu au atamzuia Afisa au Mkurugenzi kufanya kazi yake kulingana na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na hivyo atafikishwa mahakamani na akipatikana nahatia atalipa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili.

**Uwezo wa  
Mkurugenzi  
kutoa adhabu  
kwa makosa  
hayo juu**

16. Mtu yeyote ambaye atakuwa ametenda kosa la jinai na kinyume na sheria ndogo hizi. Mkurugenzi anaweza kumwamuru mkosaji, kama atakavyoona inafaa, kulipa kiasi cha fedha mradi tu isiwe chini ya kiwango cha shilingi elfu hamsini.

**Kufutwa kwa  
sheria**

17. Kama kuna sheria yeyote ambayo inafanana na hii basi sasa imefutwa na hivyo hii ndiyo hii ndiyo itakayotumika

Nembo na mhuri wa Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji uliobandikwa kwenye sheria hii ndogo kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmasharui uliofanyika tarehe..... 2008.

**AZIMINA MBILINYI  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI WILAYA RUFIFI**

**KH. CHAUREMBO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA RUFIFI**

**NAKUBALI .....**

**MheMizengo Pinda (MB)  
WAZIRI MKUU  
JAMBURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DODOMA**

**TAREHE .....2008**